**JINA:** ………………………………………… **NAMBARI:** ………………………………

**SAHIHI:** ………………………………… **TAREHE:** ……………………………….

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**102/2**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**KARATASI YA PILI**
**JULAI 2013**
**MUDA: SAA 2 ½**

# MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA NANDI KUSINI, MASHARIKI NA TINDIRET 2013

**Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari**
**KISWAHILI**
**LUGHA**
**KARATASI YA PILI**
**MUDA: 2 ½**

**MAAGIZO**

1. Andika jina lako na nambari katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
2. Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
3. Jibu maswali yote.
4. Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.
5. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma Makala Yafuatayo Kisha Ujibu Maswali.**

Teknolojia mpya ni tawi la maarifa linalohusiana na sayansi kwa upande mmoja na uhandisi (uinjinia) kwa upande mwingine. Sayansi ni elimu inayotokana na uchunguzi na majaribio katika maabara. Nao uhandisi ni ujuzi wa kuunda mitambo. Maarifa ya sayansi yaapotumiwa kutengeneza vitu viwandani hali hii inakuwa teknolojia.

Zao mojawapo la teknolojia mpya ni simu tamba. Watu vijijini sasa wanawasiliana na jamaa zao walio mbali. Akina nyanya wanapopanda njugu, kupalilia migomba, kukama ngamia au kukuna nazi, wanaweza kuzungumza na wajukuu wao walio Uingereza, Uchina au kwingine kule.

Hakuna mahali ambapo hapajafikwa na teknolojia mpya. Tukitembelea baadhi ya nyumba tutaona vifaa kama vile tanuri la miale au maikrowevu ambalo linapika maharagwe yakaiva kwa dakika chache tu. Majokofu nayo yanatuwezesha kuhifadhi vyakula bila kuharibika. Hata maiti na mizoga inaweza kuhifadhiwa kwa miaka mingi kwa ajili ya utafiti bila kuoza katika ufuo au mochari.

Kwa upande wa kilimo, teknolojia imefanya makubwa. La kustaajabisha ni mtu mmoja kulima eneo kubwa la shamba kwa trekta. Halafu akapanda kwa tandazi, Kunyunyizia dawa kunyausha magugu, akavuna na kukoboa mahindi akiwa peke yake. Siku hizi inawezekana kukuza mimea na kufuga wanyama wanaokomaa kwa muda mfupi na kutoa mazao maradufu kwa sababu ya teknolojia mpya.

Teknolojia imewezesha watu kuvumbua aina nyingi za nishati. Badala ya kutegemea umeme unaotokana na maji tu, sasa watu wanatumia mvuke, nguvu za upepo na nishati ya jua kupata umeme. Kwa sababu hii hata mababu zetu vijijini wanatazama televisheni bila shida wala wahka.

Kwa upande mwingine, teknolojia ina madhara yake. Kwa mfano, uundaji wa silaha kali unaendelea kuwaangamiza watu wengi. Mabomu ya kitonoradi yaliyoangushwa Hiroshima na Nagasaki Japan mwaka wa 1945 ni zao la kisayansi. Haya yaliwaua watu wengi na madhara yake bado yanadhihirika hata leo katika maumbile ya watoto wanaozaliwa na upungufu. Tena magaidi na wahalifu wa kimataifa wanatumia teknolojia mpya kuimarisha mbinu zao za kutenda maovu. Isitoshe, inawezekana kutumia teknolojia kuagiza benki kutuma pesa nje ya nchi bila mwenye hazina kujua.

Wahalifu wanaweza kusikiza mawasiliano ya watu kwa simu hata ikiwa ni baina ya polisi. Kisha matatizo mengi ya kiafya yasemekana yanatokana na vyakula vilivyokuzwa kutumia teknolojia mpya.

Katika usafiri, kuna garimoshi lenye kutumia stima badala ya makaa. Hili ni zao la teknolojia mpya vile vile. Ingawa mwendo wake ni wa kasi, kasi hiyo na stima huweza kusababisha ajali mbaya mno.

Ingawa madhara yapo lakini manufaa ya teknolojia ni mengi zaidi kuliko madhara yenyewe. Faida ni kuwa teknolojia hurahisisha shughuli za watu kama vile kufua na kusafiri. Pia hufanya matokeo ya shughuli kuwa bora zaidi. Kazi iliyopigwa chapa kwa kompyuta huwa safi na bora. Vile vile, vitu vinavyotengenezwa siku hizi ni vidogo na vyepesi lakini ni bora zaidi. Tukichukua mfano wa magari tunaona kuwa ni madogo lakini yenye muundo wa kuvutia. Tatizo tu ni ile kasi kubwa ambayo ni moja ya mambo yanayosababisha ajali nyingi.

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Gharama ya vitu vinavyotengenezwa kutumia teknolojia mpya ni nafuu. Teknolojia hii inatumia malighafi ya kisasa na hivyo kuhifadhi madini yetu. Pia huunda vitu ambavyo matumizi yake hayadhuru mazingira.

Tulisahau kuwa hata hapa kwetu matekinia wa Jua kali wanapiga hatua. Wanajitahidi usiku na mchana kuunda vitu vya kutuuzia kwa gharama nafuu. Mitambo ya kusukuma maji sasa inapatikana. Vyombo vya kusafirisha mizigo, vifaa vya kunyunyuzia maji, tanuri ya kuoka inayohifadhi nishati na vingine vingi, sasa vinaundwa ili kuimarisha sekta hii. Ikiimarika, Kenya inaweza kuwa nchi yenye uweo wa viwanda.

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Toa anwani mwafaka ya taarifa hii. (alama 1)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(b) Eleza umuhimu wa teknolojia mpya kwa zaraa. (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(c) "Kwa hakika uhandisi umepiga hatua." Thibitisha kauli hii kulingana na taarifa. (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(d) "Hakuna mahali ambapo hapajafikiwa na teknolojia." Unga mkono kauli hii. (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(e) Uvumbuzi wa kiteknolojia umesaidiaje ulimwengu kupunguza gharama ya uzalishaji wa bidhaa? (alama 3)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(f) Taja athari zozote mbili za kughasi za uvumbuzi. (alama 2)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(g) Taja jambo lolote linaloonyesha jinsi uvumbuzi umeibuka na anasa ya kipekee. (alama 1)

..............................................................................................................................

..............................................................................................................................

(h) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa kwenye taarifa.(alama 2)

(i) Malighafi:……………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………...

(ii) Matekinia:……………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………...

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

2. **UFUPISHO: (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata.**

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana. Akiwa na nidhamu hiyo, atakuwa mtu mwadilifu, anayeweza **kustahiwa** na kusadikika katika mambo, shughuli na hali tofauti tofauti.

Kwanza, mtoto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani mwao, shuleni na pia katika jamii. Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa **vijulanga** wote wanamtegemea kama msimamizi wa mambo **nyeti** ya maisha yao. Kwa hivyo, ni **dhahiri shahiri** kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume na mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya Idi.

Pili, huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, **mathalani** jukumu ama dhima fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani, shuleni au katika jamii. Watu hapana shaka watamteua yule mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo. Ndio maana viranja wanaoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambao tayari wamekwisha tiliwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadilifu daima atajiepusha na shutuma na majanja yote yanayoweza kuchipuka. Kuna msemo maarufu, kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu, kwamba "aliye kando haangukiwi na mti." Pia waliambiwa kwamba, "pilipili usiyoila yakuwashiani?"

Ni bayana kutokana na misemo hiyo miwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuwakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya 'watoro' ambao ni watovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozo na mielekeo ya watu wazima ambao wako mazingirani mwake. Ndipo wakale wale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.

Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbani hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kufikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu wote katika maisha yake. Ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.

Kwa vile ni bayana kwamba mabaya yote ayatendayo duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani, watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu. Ni kheri mja kujihidi mwenyewe, kwani uhalifu haulipi chochote.

(a) Nini umuhimu wa nidhamu? (maneno kati ya 50-55) (al. 1 ya mtiririko) (alama 6)

**Matayarisho**

....................................................................................................................

....................................................................................................................

....................................................................................................................

....................................................................................................................

....................................................................................................................

....................................................................................................................

..........................................................................................

**Jibu**

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

(b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (tumia maneno 55-60) (alama 1 mtiririko) (alama 7)

**Matayarisho**

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

**Jibu**

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Taja sauti yenye sifa zifuatazo: (alama 2)

(i) Mbele, juu, tandazwa: ……………………………………………………………

(ii) Kikwamizo, sighuna cha ufizi: …………………………………………………

(b) Onyesha umoja au wingi wa ngeli za nomino zifuatazo. (alama 2)

(i) Bawabu:………………………………………………………………………………

(ii) Nyasi: ………………………………………………………………………………

(c) Eleza matumizi mawili ya alama za mtajo na utolee mifano. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(d) Tofautisha matumizi ya 'vizuri' katika sentensi hii. (alama 2)

Mwalimu alivaa <u>vizuri</u> alivyofunga <u>vizuri</u>.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(e) Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama 1)

KKKI

……………………………………………………………………………………

(f) Tunga sentensi kudhihirisha matumizi mawili tofauti ya kiambishi –ji- (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(g) Bainisha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentesi ifuatayo:

Mjakazi aliwapelekea wageni chakula kwa sinia. (alama 3)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(h) Ainisha viambishi katika sentensi hii. (alama 2)

Sitakupiga

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

…………………………………………………………………………………………

(i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi. (alama 4)

Mama mzazi amepanda uchagani.

(j) Andika kwa msemo wa taarifa, "Sitathubutu kumpa kitabu changu." Chesebe alisema. (alama2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(k) Nini maana ya kiwakilishi? (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

(l) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo.

Tulibeba maji ya kutosha tulipoenda safari Turkana. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(m) Ainisha mofimu hizi; (alama 2)

i. Kunguni…………………………………………………………………………

ii. Mgeni…………………………………………………………………………

(n) Tunga sentensi katika wakati usiodhihirika. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………

(o) Kanusha bila kutumia 'amba' (alama 2)

Nitamtuza mwanafunzi ambaye ni nadhifu.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(p) Tunga sentensi ya vitenzi sambamba ukitumia vitenzi vifuatavyo: (alama 2)

Wahi, kwenda, soma

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(q) Andika katika kauli ya kutendesha. (alama 1)

Toa ushuru wa fordhani.

…………………………………………………………………………………………

(r) Eleza tofauti baina ya sentensi hii. (alama 2)

Ningekuwa na pesa ningenunua gari.

Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari.

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

(s) Sahihisha sentensi hii (alama 1)

Mwizi mwenye ameshikwa atafikishwa katika mahakamani.

……………………………………………………………………………………………..

(t) Andika maana mbili zinazotijokeza katika sentensi hii. (alama 2)

Jua nisemalo ni muhimu kwetu.

..................................................................................................................................

……………………………………………………………………………………………..

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

4. **ISIMU JAMII (ALAMA 10)**

Okoa mapesa chungu mbovu. Usidanganywe na miigizo. XYZ ndiyo tu dawa ya kipekee iwezayo kuponya zaidi ya magonjwa ishirini kwa safari moja.

(a) Taja muktadha wa sajili hii. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….

(b) Eleza sifa zozote **nne** za sajili. (alama 8)

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………